**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**HOTUBA YA MGENI RASMI, MKUU WA MKOA WA IRINGA**

# UFUNGUZI WA KIKAO KAZI NA WAANDISHI WA HABARI JUU YA UTEKELEZAJI WA SHERIA YA DAWA NA VIFAA TIBA, SURA 219

**TAREHE 16 MEI, 2024**

- **Mganga Mkuu wa Mkoa,**
- **Mkurugenzi Mkuu wa TMDA,**
- **Wakurugenzi wa TMDA,**
- **Wahariri wa vyombo vya Habari,**
- **Wageni waalikwa,**
- **Mabibi na Mabwana.**

Awali ya yote napenda kuushukuru uongozi wa Mamlaka ya Dawa na Vifaa tiba (TMDA) kwa kuona umuhimu na kunipa nafasi ya kuwa mgeni rasmi katika kufungua kikao kazi hiki muhimu cha Wahariri na Waandishi wa vyombo mbalimbali vya habari kutoka mikoa ya Iringa, Singida na Dodoma.

Nichukue fursa hii pia kutoa shukrani zangu za dhati kwa washiriki wote wa kikao kazi hiki ambayo naamini wengi mnatoka nje ya mkoa wa Iringa, kwa kuacha majukumu yenu muhimu na kukubali kushiriki katika kikao hiki. Hiki ni kielelezo tosha kuwa mnayapa umuhimu masuala yanayohusiana na usalama, ubora na ufanisi wa dawa, vifaa tiba na vitendanishi.

**Ndugu washiriki,**

Serikali ya Tanzania katika jitihada za kuboresha utoaji huduma imekuwa ikishirikisha wadau na wananchi katika shughuli zake mbalimbali ili kufikia matarajio ya jamii katika sekta ya afya. Mojawapo ya mikakati katika programu hiyo ni pamoja na vikao kazi kama hivi vya kujadili mikakati mbalimbali ya kulinda afya ya wananchi.

TMDA tangu kuanzishwa kwake. Takriban miaka 21 sasa, imekuwa ikishirikisha wananchi na wadau katika shughuli za udhibiti wa ubora, usalama na ufanisi wa dawa, vifaa tiba na vitendanishi nchini ili kulinda afya ya jamii.

**Ndugu washiriki,**

Tofauti na bidhaa nyingine, dawa, na vifaa tiba ni bidhaa nyeti na zenye madhara makubwa ya kiafya ikiwa hazikudhibitiwa ipasavyo na yanaweza kusababisha ulemavu, kupoteza maisha na hivyo kudhoofisha uchumi wa nchi. Kwa hiyo bidhaa hizo zinahitaji kudhibitiwa kwa utaratibu wa namna ya pekee; lengo likiwa ni kuzuia madhara kwa watumiaji. Katika kufikia lengo hilo bidhaa hizi zinahitaji kuhakikiwa usalama, ubora na ufanisi kabla ya kuruhusiwa kutumika, kazi ambayo inasimamiwa na TMDA.

**Ndugu washiriki,**

Baadhi ya majukumu ya msingi ya taasisi hii katika kuhakikisha afya ya wananchi inalindwa ni kufanya ukaguzi wa mara kwa mara ili kuhakikisha kuwa bidhaa zilizopo katika soko ni salama na zenye ubora. Lakini pia ina jukumu la kudhibiti matangazo ya bidhaa za dawa, na vifaa tiba ili kuzuia matangazo yenye nia ya kupotosha umma kwa lengo la kibiashara.

**Ndugu washiriki,**

Napenda kuwaeleza kuwa suala la kudhibiti matangazo ni la kisheria na katika kuhakikisha utekelezaji wake, zipo Kanuni za Udhibiti wa Matangazo ya Dawa na Vifaa tiba zilizoandaliwa chini ya Sheria Sura 219 na zilianza kutumika tangu mwaka 2010. Hata hivyo, kati ya changamoto kubwa ambazo Mamlaka imekuwa ikikabiliana nazo toka kuanzishwa kwake ni kushuhudia kutolewa kwa matangazo ya bidhaa inazozidhibiti kupitia vyombo mbalimbali vya habari bila kibali cha TMDA kinyume na matakwa ya Sheria na Kanuni na hivyo kuchangia kupotosha jamii.

**Ndugu washiriki,**

Pamoja na upungufu huu kwa vyombo vya habari, napenda nitambue ushirikiano ambao umeendelea kutolewa na baadhi ya vyombo vya habari ambavyo vimekuwa vikitoa taarifa kwa Mamlaka juu ya ukiukwaji wa sheria hususan urushwaji wa matangazo bila kibali cha TMDA.

Aidha, napongeza vyombo vya habari, wahariri na waandishi ambao wamekuwa wakitoa taarifa mbalimbali kuhusu umuhimu wa kudhibiti bidhaa unaofanywa na TMDA na hivyo kuongeza uelewa wa Jamii.

Ni kwa kuzingatia umuhimu wenu na michango yenu ndio maana tunakutana leo hii ili tuweze kujadiliana kwa pamoja na kutoa maoni ambayo yataisaidia TMDA kuboresha huduma zake na hivyo kufanikisha lengo kuu la kulinda afya za watumiaji wa bidhaa hizi ambao kimsingi ni sisi wenyewe pamoja na familia zetu, ndugu, jamaa, majirani na marafiki.

Mamlaka ya Dawa na Vifaa tiba haiwezi kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi bila ushirikiano wenu. Ni imani yangu kuwa kwa kufanya kazi kwa ushirikiano na kushirikisha wananchi mtaweza kuelewa matatizo yaliyopo katika jamii yanayohusiana na usalama na ubora wa bidhaa zinazodhibitiwa na TMDA na hivyo kuwa na mchango mkubwa katika kuhakikisha kwamba Sheria ya Dawa na Vifaa tiba Sura 219 inatekelezwa na wadau wote kwa ufanisi.

**Ndugu washiriki,**

Mtakumbuka hivi karibuni, TMDA imekuwa ikitoa taarifa kwa umma kuhusu uwepo wa dawa duni na bandia mbalimbali katika nchi yetu. Uwepo wa dawa hizi bandia ni hatari sana kwa afya za wananchi. Hivyo, ninawaomba sana mkaendelee kutumia vyombo vyenu kuwaelimisha wananchi kuhusu suala hili hususan kuwaelimisha wananchi waache mara moja kununua dawa zinazotembezwa mikononi ikiwa ni pamoja na katika vyombo vya usafiri kinyume cha Sheria kwani mara zote dawa hizo huwa ni duni au bandia. Serikali haitamwonea huruma mtu yeyote atayepatikana na dawa bandia kwa kigezo kuwa hawakujua kwamba ni bandia wakati huo huo akiwa amesababisha madhara kwa wagonjwa.

**Ndugu washiriki,**

Nawaombeni sana muendeleze ushirikiano ambao mmekuwa mkiutoa kwa TMDA katika kuelimisha juu ya udhibiti wa bidhaa na matumizi sahihi ya dawa na vifaa tiba hususan kupitia matumizi ya kalamu na sauti zenu. Kupitia kwenu jamii imeweza kuifahamu TMDA na kazi zake na hivyo kuweza kutoa taarifa pale wanapotilia mashaka na ubora

na usalama wa bidhaa za dawa na vifaa tiba vilivyopo katika soko ili hatua stahiki ziweze kuchukuliwa.

Ni matumaini yangu kwamba mtasikiliza na kuchangia mada zitakazotolewa na hatimaye mtaainisha changamoto zilizopo katika kudhibiti usalama na ubora wa bidhaa husika. Kufuatia changamoto mtakazoainisha, mtaweka mikakati ya pamoja juu ya kuimarisha udhibiti wake pamoja na udhibiti wa matangazo ya bidhaa husika ili wananchi wapate taarifa sahihi na kuweza kufanya uchaguzi wa bidhaa zenye usalama na ubora kwa afya zao.

Baada ya kusema haya machache napenda kuchukua nafasi hii kutamka kwamba kikao kazi cha Wahariri na Waandishi wa habari kutoka mikoa ya Dodoma, Singida na Iringa kuhusu utekelezaji wa Sheria ya Dawa na Vifaa tiba Sura 219 yamefunguliwa rasmi.

**ASANTENI KWA KUNISIKILIZA**

---

**MWISHO**